# MUDA UMEWADIA
# WA MKATABA MPYA WA KIJAMII



# ENEZA UJUMBE

**Eleza marafiki na wafuasi wako kuhusu nguvu za Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu kisha uwahimize walitumie.**

**#Timefor8**

**Sambaza taarifa unayoipendelea kuhusu ukuzaji wa #Timefor8 katika tovuti yako pamoja na mitandao ya kijamii.**

**www.timefor8.org**

Kutwaliwa kwa Ajenda 2030 pamoja na Malengo yake ya Maendeleo Endelevu kunaashiria fursa ya kihistoria ya kubadilisha namna ulimwengu unavyofanya kazi.

Katika vyama vya wafanyakazi, haki za kijamii, kiuchumi na kimazingira ambazo ni nguzo ya Malengo ya Maendeleo Endelevu ni muhimu mno kwa ajenda ya ajira.

Na kupitia kazi yetu ya kila siku-kuweka kipau mbele uhuru wa kutangamana na mazungumzo ya kijamii, majadiliano ya pamoja na kulinda haki za wafanyakazi-vyama vya wafanyakazi huchangia mno katika kutimiza Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Lengo la Maendeleo Endelevu la 8 linalenga kuendeleza ukuzaji endelevu wa kiuchumi kwa watu wote, pamoja na ajira bora kwa watu wote. Lengo hili ni muhimu mno katika muundo wa Ajenda 2030, na ni la kimsingi katika mwito wetu wa Mkataba Mpya wa Kijamii kati ya serikali, biashara na wafanyakazi.

**Ni wakati wa 8 Muda umewadia wa Mkataba Mpya wa Kijamii.**



## UHURU WA KUJIUNGA NA CHAMA HUKUPA NAFASI BORA YA KUTETEA HAKI YAKO YA UJIRA BORA NA MAZINGIRA BORA YA KAZI.

Ili kuhakikisha kuwa ajira bora imefanyika sheria, na kwamba mamilioni ya familia za wafanyakazi wanaepuka umaskini na unyanyasaji, wafanyakazi wanastahili kupewa uwezo wa kuwa na ushawishi katika uamuzi utakaoathiri maisha yao. Ni sharti watu wawe na uwezo wa kushirikiana(uhuru wa kushirikiana) kupitia vyama vya wafanyakazi ili wapate kujadili ujira na kutetea mazingira bora ya kazi kwa kiwango sawa na waajiri wao(mazungumzo ya pamoja).

Kuna sheria mbili kuu kuhusu swala hili zinazotambulika kimataifa- Mapatano ya Shirika la Kimataifa la Ajira 87 na 98. Inasikitisha kuwa mataifa mengi na waajiri hukaidi sheria hizi na hivyo kusababisha ukosefu wa usawa huku wafanyakazi wakiteseka bila sababu.

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu linanuia kuhakikisha kwamba hakuna anayewachwa nyuma ulimwengu unapochukua mwelekeo wa njia endelevu zaidi za kuishi na za ajira.




**ULAFI WA KISHIRIKA HAUTAKOMESHWA PASIPO SHERIA DHAHIRI ZINAZOSTAHILI KUFUATWA NA MASHIRIKA YA KIMATAIFA PAMOJA NA UWEPO WA MIUNGANO YENYE NGUVU YA KUZITEKELEZA SHERIA HIZO.**

Mahali ajira bora ni jambo la kawaida, wafanyakazi hushughulikiwa kwa njia ya heshima. Lakini siku hizi, mamilioni ya wafanyakazi wananyanyaswa kwa sababu ya ulafi wa kishirika. Mashirika ya kimataifa yanazidi kutajirika kutokana na muundo wa kiuchumi unaoshinikiza ongezeko la uzalishaji kwa kupunguza bei huku wafanyakazi wakikandamizwa.

Ni wajibu wa mashirika kuhakikisha kuwepo kwa hali bora ya wafanyakazi wanaotengeneza bidhaa zao pamoja na watu wanaozitumia. Makampuni yana wajibu wa kujua kinachoendelea katika ugavi wao(uangalifu), huku serikali zikihakikisha kuwa mashirika yanafuata sheria. Mashirika ya wafanyakazi hutekeleza jukumu kuu katika kuhakikisha kuwa pande zote mbili zimewajibika.

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu linalenga kuhakikisha kuwa kuna umoja kati ya mashirika, serikali na vyama vya wafanyakazi katika kujenga ulimwengu endelevu ambao hautamwacha yeyote nyuma.

**KUPATA NAFUU BAADA YA KUUGUA, KUJUA KUWA UNAOWAPENDA WAMELINDWA VILIVYO UNAPOFANYA KAZI, KUFURAHIA MIAKA YAKO YA BAADAYE- KUNA SABABU NYINGI ZA KUUNGA MKONO ULINZI WA KIJAMII KWA WATU WOTE.**



"Kila mmoja wetu hupitia vipindi ambavyo anahitaji msaada zaidi. Lakini watu wengi hawapati ulinzi wa kijamii unaofaa. Ajira bora ni zaidi ya maisha yetu ya kazi ya kawaida. Pindi tunapostaafu, tunatarajia kupokea malipo ya uzeeni ili tufurahiye maisha ya baadaye. Iwapo tuna watoto, tunataka tuendelee kufanya kazi tukiwa na hakikisho kuwa tunaowapenda wamelindwa vyema. Na iwapo kutatokea ajali au ugonjwa, tutahitaji kulipia gharama zetu; aidha, tutahitaji huduma bora za afya bila kuzingatia mapato yetu."

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu linahusu kutoa huduma bora za kijamii kwa watu wote.



**VYAMA VYA WAFANYAKAZI VINACHANGIA PAKUBWA KATIKA KUHAKIKISHA KWAMBA HAKUNA MFANYAKAZI ANAYEWACHWA NYUMA KATIKA MPITO WA KUELEKEA KWENYE SIKU ZA USONI ENDELEVU.**

Ulimwengu hauwezi kuendelea na hali ilivyo sasa. Tamaa mbaya ya mashirika ya kimataifa yenye uchumi unaozidi kukua kila uchao kwa sababu ya matumizi yasiyokuwa na kikomo inaelekeza binadamu kwenye Mwisho mbaya usio na njia ya kutoka. Ni wakati wa ruwaza mpya itakayotuwezesha kufurahia siku za usoni endelevu zenye msingi wa ajira bora. Kwa sababu baadhi ya kazi zitachukua sura mpya au zingine mpya kuchukua nafasi ya zile za awali, wafanyakazi watalazimika kupokea ujuzi na msaada watakaohitaji katika huu ulimwengu mpya wa kazi.

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu linahusu kubadilisha namna tunavyoishi, kufanya kazi na kuzalisha ili kuhakikisha kuwa kuna siku za usoni endelevu kwa manufaa ya vizazi vijavyo.

**WANAOFANYA KAZI ZISIZO RASMI HUZALISHA MALI KUTOKANA NA UMASKINI WANASTAHILI KUPATA AJIRA RASMI ZENYE HAKI SAWA NA ZILE ZA WAFANYAKAZI WENGINE.**



Kwa mamilioni ya watu ulimwenguni wanaofanya kazi katika sekta ya uchumi usio rasmi, ajira bora huwapa tu matumaini ya siku bora za usoni. Licha ya kupambana kwao kila siku ili kuweza kujikimu, wengi wa wafanyakazi wasio rasmi hawana mapato thabiti, hawana muda wa kufanya kazi uliothibitiwa, hawana malipo ya uzeeni, hawana usalama wa kijamii, hawana bima ya afya, wala hawana namna ya kuepukana na hali yao. Ingawa wanazalisha mali kutokana na umaskini na pia hao ndio injini ya uchumi halisi katika maeneo mengi ulimwenguni.

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu linahusu kuhakikisha kuwa wafanyakazi wana ajira rasmi na uwezo kamili wa kupata haki zao.



**IWAPO UNA KAZI, MAPATO YAKO YANAPASWA KUWA YA KUTOSHA ILI KUKUWEZESHA KUWA NA MAISHA YANAYOHESHIMIKA.**

"Katika ulimwengu wenye mpangilio usioweza kudumishwa ambapo pana uhaba wa ajira bora, kuwa na ajira hakulinganishwi na kuishi maisha ya kuheshimika. Kwa upande mwingine, idadi ya wale wasioweza kukimu mahitaji yao licha ya kuwa na ajira moja au kadhaa inazidi kuongezeka.

Ujira wa chini zaidi katika maisha unawapa mamilioni ya wafanyakazi na familia zao fursa ya kuondokea umaskini. Tunastahili kuwa na uwezo wa kuthibiti maisha yetu tena na kunawiri katika kazi zetu na katika jamii zetu. Vyama imara vya wafanyakazi na kuipa sheria nguvu ni vipengele muhimu katika kutekeleza swala hili."

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu ni kuhakikisha kuwa iwapo mtu ana ajira anapata ujira bora utakaomwezesha kuishi maisha ya kuheshimika.



**VYAMA VYA WAFANYAKAZI VINAPOKUWA NA VIKAO, MASHIRIKA MAKUU PAMOJA NA SERIKALI HUWEZA KUSAIDIWA ILI KUUNDA SERA NA TARATIBU ZINAZOHUSISHA WATU WOTE.**

"Tangu jadi majadiliano kati ya serikali, waajiri na vyama vya wafanyakazi huhusu mishahara na mazingira ya kazi. Kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi na teknolojia, majadiliano haya sasa yameanza kuhusisha hatua zinazopaswa kuchukuliwa ili kuhakikisha kwamba hakuna atakayewachwa katika harakati za mpito wa jamii kuelekea kwenye siku za usoni endelevu. Kama wanaopigania ajira bora, vyama vya wafanyakazi huwa mstari wa mbele katika kutetea haki na heshima kwa wafanyakazi."

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu linahusu kuwawezesha wafanyakazi kuchangia katika uamuzi utakaoathiri maisha yao.



**ULAFI UMEPELEKEA ULIMWENGU KUKARIBIA KUPOROMOKA KATIKA SEKTA YA MAZINGIRA NA JAMII. TUNAHITAJI MKATABA MPYA WA KIJAMII HARAKA ILI KUHAKIKISHA KUWA HAKI ZINAHESHIMIWA NA MASHIRIKA KUWAJIBIKA.**

Ni sharti nguzo za kimsingi za ulimwengu endelevu kama vile ajira bora ziwe za kudumu. Ndio maana tunapendekeza kuundwa kwa Mkataba Mpya wa Kijamii.

Mfumo huu utafafanua kinaga ubaga majukumu ya washikadau wote katika jamii, kama vile serikali, waajiri na wafanyakazi, pamoja na haki zao. Kwa wafanyakazi, hii inahusu haki za kimsingi za ajira zilizojumuishwa katika dhamana ya ajira kwa watu wote: uundaji wa vyama; kuhusika katika majadiliano na waajiri(mazungumzo ya pamoja); hakikisho la mapato ya kutosha; kuzuia ubaguzi na unyanyasaji; kufurahia mazingira bora ya kazi; na kuwa na uwezo wa kutosha wa kuthibiti muda wa kufanya kazi.

Lengo la 8 la Maendeleo Endelevu linahusu kuuwezesha ulimwengu kuanza njia mpya endelevu ya kuishi chini ya ulinzi dhidi ya ulafi ambao unatuelekeza kwenye kusambaratika kunakotukodolea macho hivi leo.

#Timefor8
www.timefor8.org

Kwa msaada
wa Jumuia
ya Madola

ITUC CSI IGB

#Timefor8 ni kampeni ya Muungano wa Kimataifa wa Vyama vya Wafanyakazi

Responsible editor: ITUC • Boulevard du roi Albert II 5, B1 • 1210 Brussels • Belgium • dce@ituc-csi.org